# 17 USHAURI WA KIMBINGU DHIDI YA NGUVU ZA GIZA



Dunia hii tunayoishi imejaa mambo mengi ya nguvu za giza ambayo yanatufanya sisi kushangaa sana. Kuna watu ambao huzungumza na wafu, nguvu fulani zisizo za kawaida ambazo zinaweza kutenda mema ama mabaya, kama vile kuponya kimujiza, n.k. Kuna mikutano ya rohoroho ambapo wale kina kiti hupagawa na pepo; vipande vya samani hurushwa huku na kule. Kuna nyumba fulani ambazo kwa halisi hupenda kutembelewa, ambamo taa fulani huwashwa na sauti fulani za kigeni husikika kunako usiku wa manane, n.k. Kuna nguvu fulani za giza zilizowaleta watu kwenye mashaka, magonjwa na kutengana na familia, na kifo. Hata wanasiasa, wafanya biashara pamoja na watu maarufu huwaendea wale wapiga ramli. Mamilioni ya watu husoma maaguzi kwa nyota kwa kila siku, wengine wanasomewa kadi zao, lakini hawa wote hudanganywa tu. Nguvu hizi za giza hutoka wapi? Tunawezaje kulindwa dhidi ya nguvu hizo? Mungu ndiye pekee ajuaye kama kuna nini huko mbele. Ameyafunua haya katika nabii za Biblia zipatazo 2,300. Wapiga ramli wanayajua ya wakati huu na ya wakati uliopita, na jambo hili huwaingia watu moyoni; hii ni kwa sababu wanafanya kazi pamoja na pepo ambao sisi hatuwezi kuwaona, lakini hata hivyo wako upande wetu. Hawa ni pepo wale wale wanaotokea katika mikutano ya rohoroho. Isaya 8:19.

## *NGUVU HIZI ZA AJABU NI NANI?*

**1. Je, hizi zitakuwa ni roho za wafu? Biblia inasemaje juu yao waliokufa? Mhubiri 9:5, 6.**

____________________________________________________________

**2. Je, yawezekana kwamba Mungu ndiye anayewaongoza hawa? Ni amri gani Mungu aliyotoa? Walawi 20:27; Kumbukumbu 18:10-12.**

____________________________________________________________

**3. Iwapo mafunuo haya hayaji kutoka kwa Mungu wala kwao waliokufa, ni nani anayewahamasisha wanasiasa? Ufunuo 16:14.**

____________________________________________________________

a) Roho hizi za mapepo ni wale malaika walioanguka ambao walimwasi Mungu (Ezekieli 28:13-18).

b) Theluthi moja ya malaika walifukuzwa kutoka mbinguni (Ufunuo 12:9, 12).

**4. Katika mifano ya Kibiblia juu watu waliopagawa na pepo, wale pepo walisema nini bayana? Matendo 16:16-18. Weka alama katika jibu sahihi:**

☐ Walisema uongo

☐ Walisema mambo yasiyo na maana

☐ Mlikuwamo na ukweli katika yale waliyoyasema.

**5. Kulitokea nini kwa Mfalme Sauli pale alipokwenda kwa wapiga ramli baada ya Mungu kumkataa? 1 Samweli 28:3, 6 - 8, 11-15; 1 Nyakati 10:13, 14.**

____________________________________________________________

## *HALAIKI YA PEPO*

**6. Ishara ya siku za mwisho ni ipi? 1 Timotheo 4:1.**

______________________________________________________________

a) *Sio Wana-rohoroho wenye mfumo pekee ndio waliopo, bali pia kuna wachawi na waaguaji; hawa pia wamejipenyeza katika makanisa ya Kikristo.*

b) *Kiti wa kwanza aliyepata kutumiwa alikuwa ni nyoka (Mwanzo 3:1-4). Viti wengine ni watu wengine ambao huingia katika hali kama ya usingizi mzito na kisha wale pepo huongea kwa kupitia kwao. Wanajifanya kuwa wanaweza kuwafanya wafu waongee, kuvisogeza vitu pasipo kuvigusa, kuponya wagonjwa, kutoa ujumbe, n.k.*

**7. Twawezaje kusema ukweli kutoka kwenye makosa? Isaya 8:19, 20.**

*Mjumbe wa Mungu ataafikiana na* ____________________ *na* ___________________ *katika kila jambo; ni lazima akubaliane na kile ambacho Mungu amekithibitisha huko nyuma kupitia kwa neno Lake.*

**8. Je, Biblia inasema nini juu ya wale wanaotafuta ufumbuzi wa matatizo yao kutoka katika nguvu hizo za giza? Yeremia 2:13.**

______________________________________________________________

a) Kwa misemo ya siku hizi, tunazungumza juu ya Parapsychology. Kuna watu ambao hupita kati ya moto bila ya kuungua nao husema ya kwamba wanaweza kufanya hivyo kutokana na nguvu za kiakili. Jambo hili Mungu alililikataza (Kumbukumbun18:9-14).

b) Kusoma viganja ni kuagua.

c) Kumtia mtu usingizi na kumwamrisha kimazingara, pamoja na kuponya kwa njia ya maneno ya kiganga, hata kama imefanywa kwa nia njema, Mungu hajazikubali.

**9. Je, Biblia inasemaje juu ya wale wanaofanya falaki na kuwauliza wanajimu? Isaya 47:13-15.**

______________________________________________________________

**10. Katika siku za mwisho, miujiza ya uongo itakuwa udanganyifu ambao utawapoteza hata ______________________________. Mathayo 24:24.**

*Kuna mambo ambayo pengine huwezi kuyaona kuwa ni mabaya sana, lakini yanaweza kuvifikia viwango vya yale Mungu asiyoyapenda; na hata kama huwezi kuliamini hili, wewe unaongozwa na nguvu fulani zilizofichika. Ni jambo bora zaidi kuachana na mambo yote ya jinsi hii.*

**11. Je, Shetani hutenda kazi yake bure, ama kama anatoza kwa ajili ya "hisani" zake? Warumi 6:16; Yohana 8:44.**

______________________________________________________________

*Shetani hulipisha kwa bei kubwa kwa wale wanaomwendea ili kushauriwa naye. Mtu huyo aweza kuletewa:*

- *Kutokuamini, mashaka, kupoteza imani juu ya neno la Mungu pamoja na sala.*
- *Msongo, wasiwasi, na hata kujaribu kujiua.*
- *Magonjwa ya kiakili, kuchanganyikiwa kiakili,*
- *Mapotofu ya kijinsia, uzinzi, ulevi, ughaibu wa madawa ya kulevya.*
- *Hasira isiyotawalika. Kupagawa na mapepo. Magonjwa, umaskini, nakadhalika.*

*Baada ya kuomba msamaha wa Mungu kwa ajili ya kushauriana na watu kama hawa ama kwa kutafuta usaidizi kutoka kwa watu mbalimbali zaidi ya Mungu, amua sasa kutofanya hivyo tena.*

**12. Je, vile vitabu vya uganga pamoja na vitu vingine vya jinsi hii vifanyiwe nini? Matendo 19:19.**

________________________________________________________________

**13. Je, ni ushauri gani wa kimbingu ambao utatuweka huru kutokana na ile mivuto ya kishetani? Yakobo 4:7.**

*a) ________________________________ Mungu.*

*b) Kumpinga __________________________ . Kutomsikiliza wala kumwamini.*

*c) Shetani ________________________________________________ .*

**14. Je, tutumainie nini ili kupata ushindi kamili? Ufunuo 12:10, 11.**

________________________________________________________________

## *HITIMISHO*

- Pale Adamu na Hawa walipojitenga na Mungu, waliahidiwa ya kwamba Kristo atamshinda Shetani na kumponda kichwa chake (Mwanzo 3:15). Jambo hili lilitokea pale katika kifo cha Yesu.
- Yesu anataka kukutetea, kukusaidia, kukusamehe, na kukuficha wewe katika mikono Yake yenye upendo.

**15. Baada ya kumweka huru yule Mgerasi (Luka 8:26 -28), je, ni ushauri gani ambao Yesu alimpatia? Luka 8:38 39.**

________________________________________________________________

***Uamuzi wangu:*** *Ninaamini ya kwamba tunapasa kutafuta msaada kutoka kwa Yesu; sio kwa waonaji, waponyaji, wanajimu ama watu wa rohoroho.* ○ *Ndio* ○ *Hapana*